**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Pia, nachukua nafasi hii adhimu kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na weledi wa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyoiongoza nchi yetu na hatua mbali mbali anazozichukua katika kukuza sekta ya kilimo kwa kutoa mchango mkubwa wa fedha za maendeleo ya miradi mbali mbali ambayo kukamilika kwake kutawanufaisha wananchi wetu moja kwa moja. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa mchango mkubwa wa muongozo na mawazo wanaompatia Rais wetu juu ya jinsi ya kuiongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo na mabadiliko chanya katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia inachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Dr. Soud Nahoda Hassan kwa mashirikiano yake makubwa aliyoipatia Kamati hii katika kipindi chote cha uongfozi wake, tunamtakia kila la mkheri katika majukumu yake ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa ushiriki wao mzuri wakati wa kupitia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, jambo linalonitia moyo wa kutekeleza na kusimamia majukumu tuliyopangiwa kwa mujibu wa kanuni zilizopo,

hasa tukizingatia kwamba Kamati hii inasimamia masuala muhimu ambayo yanagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya wananchi katika harakati zao za kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uwasilishwaji wa makadirio ya mapato na matumizi Kwa Wizara tunazozisimamia, wajumbe hawa walionekana kuwa makini sana katika kutoa michango, maoni na ushauri ambao utaweza kusaidia katika utekelezaji wa malengo yaliyopangwa kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena niwatambue wajumbe pamoja na makatibu wetu wa Kamati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yussuf Hassan Idd | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Aza January Joseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Salum Nassor Ali | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Said Swaleh Salim | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 8. | Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kulitekeleza jukumu la msingi lililoelekezwa katika Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020), la kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kila mwaka wa fedha, ilikutana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kwa lengo la kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nifafanue kidogo Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Wizara hii, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 4.00 kupitia vyanzo vyake kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia mwezi Machi 2022, Wizara ilifanikiwa kukusanya shilingi bilioni 3.160 ikiwa ni sawa na 79% ya makisio hayo. Kamati imebaini kuwa, vyanzo vya mapato kwa Wizara ya Kilimo vikisimamiwa ipasavyo vinauwezo wa kukusanya mapato katika kiwango kukubwa kutokana na uwezo wa vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na ukusanyaji wa kuridhisha uliofanyika, Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara kwa kukusanya makusanyo mazuri

pamoja na changamoto kadhaa ambazo Wizara ilikumbana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kuvisimamia vyema vyanzo vyake vya mapato, ili viweze kutoa tija zaidi na kuyafikia malengo yaliyowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Matumizi, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 53.70, na hadi kufikia mwezi Machi 2022, Wizara imefanikiwa kupata shilingi bilioni 23.66. Kamati inasikitishwa sana na kiwango kidogo cha fedha iliyopatiwa Wizara hii kwa kipindi hicho, hali inayopelekea changamoto kadhaa kwa Wizara katika kutekeleza majukumu iliyojipangia ikiwa ni pamoja na kusuasua kwa miradi kadhaa ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imepangiwa kutekeleza programu kuu nne (4) kama ifuatavyo:

i) Programu kuu ya Maendeleo ya Kilimo;

ii) Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;

iii) Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo;

iv) Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Mheshimiwa Spika, Programu hii utekelezaji wake unahitaji fedha za kutosha hasa tukizingatia kuwa, programu imekusanya mambo mengi sana ambayo ni ya msingi katika kuiletea nchi yetu maendeleo. Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii imeshangazwa sana kuona fedha iliyokadiriwa kwa mwaka huu wa fedha ni ndogo sana ukilinganisha na bajeti iliyopita. Jumla ya shilingi 34,087,798,000 zimekadiriwa kutumika kwa programu hii kwa mwaka huu wa fedha ambapo shilingi 37,308,868,000 zilipangwa kutumika kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupitia bajeti ya programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa chakula kupitia huduma ya kuimarisha Upatikanaji wa pembejeo za kilimo, ilisikitika sana kuona huduma hii muhimu kwa wakulima wetu haikutengewa fedha yoyote. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, kwa sasa Serikali imeamua kuondoa kabisa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima. Aidha Kamati katika ziara zake ilizozifanya ilibaini kuwa, kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa pembejeo hizo kwa wakulima hao, ambapo kukosekana kwake kunazorotesha uzalishaji ulio bora.

Mheshimiwa Spika, tukirejelea hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati akilifungua Baraza la Wawakilishi mwezi Novemba 2020, tutakumbuka kwamba, moja katika mambo muhimu aliyoyatilia mkazo kuyatekeleza katika uongozi wake kwa Wizara hii ni ununuzi wa pembejeo za kilimo, ambazo zililenga moja kwa moja kuwasaidia wakulima wetu kuweza kulima kilimo chenye tija .

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kulifikiria upya suala la kuondoa moja kwa moja ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima wetu na kuwapatia pembejeo hizo japo kupitia njia ya mkopo, kwa lengo la kuwasaidia katika uzalishaji wa mazao yaliyo bora. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kutoa elimu ya kutosha kwa jamii juu ya matumizi ya mbolea za asili ili kuendelea na shughuli za kilimo bila ya kuathiri uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo ni moja kati ya Wizara zenye miradi mingi ya Maendeleo inayohitaji kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Umwagiliaji Maji, Mradi wa Kudhibiti Sumu Kuvu unaaotokana na ulaji wa Mahindi na Njugu Tanzania na Mradi wa Kudhibiti Nzi wa Matunda .

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati imebaini kwamba miradi mingi iliyopangwa kutekelezwa na Wizara hii, haikukamilika kutokana na usimamizi usioridhisha wa miradi hiyo. Mfano mzuri ni Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula liliopo Dodeani kisiwani Pemba. Kamati ilifanikiwa kuukagua mradi huo mara kadhaa bila ya kuridhika juu ya utekelezaji wake. Aidha Kamati ilitoa miongozo kwa Mkandarasi wa ujenzi huo kwa lengo la kuhakikisha kuwa mradi unakamlika kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika. Kwa masikitiko makubwa mradi huo hadi sasa bado haujakamilika kwa sababu ya changamoto kadhaa zitokanazo na Mkandarasi wa ujenzi huo ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo pamoja na ukosefu wa fedha kwa mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua nafasi hii kuishauri Wizara ya Kilimo, kuongeza nguvu katika kuisimamia miradi yote ya Maendeleo kwa lengo la kuiletea nchi yetu maendeleo. Aidha Kamati inashauri kuwafanyia upembuzi yakinifu *'DUE DELIGENCE'* wakandarasi wote wa ujenzi watakaoweka maazmimio ya kuiendesha miradi kwa lengo la kujiridhisha juu ya uwezo walionao katika kuiendesha miradi husika na Wataalamu wetu wasiridhike na Maandiko *'documents'* wanazowasilishiwa. Ikumbukwe kwamba, miradi hii inatumia fedha nyingi za Serikali, hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuisimamia miradi hii kikamilifu na hatimae thamani halisi ya fedha iweze kuonekana na miradi iweze kuwanufaisha wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ukweli ni kwamba, Kamati haikuridhika na kiwango hicho cha fedha kilichokadiriwa kwa Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo kutokana na shughuli nyingi na muhimu zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha na tunaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa fedha zilizokadiriwa kwa mwaka huu wa fedha zinapatikana kwa asilimia mia moja na zipatikane kwa wakati.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi **4,059,674,000** wakati mwaka wa fedha uliopita programu hii ilitengewa shilingi **2,766,841,000** Kamati inapongeza ongezeko la fedha lililofanywa na Serikali katika programu hii na inaamini kuwa mwaka huu wa fedha wananchi watashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu mbali mbali yaliyopangwa ya kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao.

**Mheshimiwa Spika**, katika bajeti iliyopita Kamati ilipokua katika ziara zake ilipata nafasi ya kuutembelea Msitu wa Uzi Ng'ambwa ulioanzishwa mwaka 2011 ambao una eka 110. Kamati ilipofika katika eneo la Msiti ilielezwa na Idara ya Misitu na Maliasili kuwa imeshindwa kuupandisha hadhi Msitu huo na kuwa Msitu wa Hifadhi kutokana na ukosefu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kuwa ongezeko hili la fedha litasaidia kuupandisha hadhi msitu huu na kuiwezesha Serikali kukusanya mapato ya utalii kupitia msitu huo. Kamati haitegemei kuja kusikia kuwa miongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele katika programu msitu huu haumo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Mifugo kwa kutenga fungu katika bajeti hii kwa lengo la kununua Mtambo mpya wa kuzalishia gesi ya kupandishia ng'ombe

wa sindano. Kamati inaamini kununuliwa kwa mtambo huo kutaongeza kiwango cha uzalishaji wa gesi na kuleta manufaa makubwa kwa wafugaji wetu. Mtambo uliopo hivi sasa umechakaa sana hali inayopelekea kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa gesi kituoni hapo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Mifugo kuutunza mtambo huo mpya utakaonunuliwa kwa kuufanyia matengenezo ya mara kwa mara *'services'* kwa wakati ili uweze kudumu kwa muda mrefu hasa tukizingatia mtambo huo ni wa gharama kubwa .

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa programu hii unaweza kusuasua kutokana na bajeti ndogo iliyotengwa kwa mwaka huu wa fedha ukilinganisha na shughuli za msingi zinazohitaji kutekelezwa. Jumla ya shilingi 6,174,784,000 zinakadiriwa kutumika, fedha ambayo ni tofauti na ile iliyopangwa kwa bajeti iliyopita ambapo ilifikia shilingi bilioni 6,947,227,000.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kwamba, matokeo ya utafiti yanaweza kutumika katika kutatua changamoto kadhaa ambazo Wizara inakabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kufanya tafiti mbalimbali na kuyatumia matokeo ya tafiti hizo katika kutatulia changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo kwa kutenga fedha za kuimarisha kitengo cha takwimu za kilimo, kitengo ambacho kitaweza kusaidia sana katika uwekaji wa takwimu zilizo sahihi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kuwajengea uwezo watendaji wote waliomo katika taasisi zake ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na waweze kuitumia mifumo iliyopo duniani katika kupata takwimu zilizo sahihi kwa maendeleo ya taifa letu.

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Niwashukuru pia Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa nilipokuwa nikiiwasilisha hotuba hii. Sasa niwaombe Wajumbe wako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kuyafanikisha na kuyatekeleza yale waliyojipangia kwa mwaka huu wa fedha unaokuja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii naunga mkono hoja hii kwa 100%.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo, **naomba kuwasilisha**.

Ahsante,

……………………………

Yussuf Hassan Idd,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.